

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE**

*Barua zote ziandikwe Kwa Mkurugenzi Mtendaji Wa Wilaya*



Kumb. Na. EA.174/302/01/100

29/09/2020

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenyе sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya **Mtendaji wa Kijiji III** na **Katibu Mahsusisi III**. Tangazo hili limetokana na Kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb. Na. FA 170/523/01'B"/15 cha tarehe 09 Septemba, 2020 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

### **1. MTENDAJI WA KIJINI – NAFASI 6**

#### **1.2 SIFA ZA MWOMBAJI**

Wahitimu wa kidato cha nne au sita waliomaliza mafunzo ya Cheti/Astashahada ya mwaka mmoja, katika moja ya fani za **Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **1.3 MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kuwa Afisa masuuli (Mhasibu) na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao
- iii. Kuwa Katibu wa Mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- iv. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu zilizopo katika kijiji
- v. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalamu katika Kijiji
- viii. Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- ix. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za Kijiji
- x. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

## **1.4 NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali ngazi ya mshahara TGS B

### **2. KATIBU MAHSUSI DARAJA III – NAFASI 1**

**2.0** Kuajiriwa kwa wahitimu wa kidato cha IV waliohudhuria Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu. Wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na Kupata cheti katika Programu za **Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.**

#### **2.1 MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- iii. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi na kumuarifu mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasadizi hao.
- vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

### **2.2 NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali ngazi ya mshahara TGS B

### **2.3 MASHARTI YA JUMLA.**

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania
- ii. Waombaji wote waambatanishe Cheti cha kuzaliwa
- iii. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi (CV) namba za simu za kuaminika na majina ya wadhamini watatu (Referees)
- iv. Waombaji waambatanishe picha 2 "Passport Size" za hivi karibuni
- v. Waombaji wote waambatanishe nakala ya vyeti halisi vya masomo na taaluma (NTA Level 5). Mwombaji atakayewasilisha (**Result Slip**), (**Provisional of Results**), au (**Statement of Results**) maombi yake hayatakubaliwa.

- vi. Kwa waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA).
- vii. Waliomaliza vyuo nje ya nchi wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Elimu ya Ufundu la Taifa (NACTE).
- viii. Waombaji watakaokidhi vigezo ndio watakaoitwa kwenye usaili (interview).
- ix. Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatashughuliwa.
- x. Waombaji wawe na umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18.


#### **2.4 MWISHO WA KULETA MAOMBI**

Mwisho wa kuleta maombi ni tarehe 12/10/2020 saa 9:30 alasiri. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P. 6,  
**MAKETE.**

Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Makete [www.maketedc.go.tz](http://www.maketedc.go.tz)

Limetolewa na;

  
David A Mgonja  
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)  
**MAKETE.**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
MAKETE**